

## **Hotuba ya Balozi katika Siku ya ITEC - 19 Machi 2019**

Mheshimiwa Naibu Katibu Mkuu wa Elimu, Sayansi, Teknoloja na Mafunzo ya Ufundii, Profesa James Mdoe

Wapendwa wangu Wahitimu wa ITEC

Mabibi na Mabwana,

Namaskar, Good evening, Habari za jioni

Karibuni sana kwenye siku ya ITEC!

Leo ni sherehe ya miaka hamsini na tano ya Mpango wa India wa Ushirikiano wa Kiufundi na Uchumi. Ushirika wa India na ndugu zetu wa Tanzania na nchi nyingine zinazoendelea ulianzishwa rasmi mwaka elfumoja miatisa sabini na nne wakati India ikifanya harakati zake kuelekea maendeleo. Hii iliwasilisha dhamira yetu ya mshikamano na kushirikiana na wenzetu wa nchi zinazoendelea kwa imani yetu imara na kujidhatiti kwetu katika ushirika wa nchi za kusini (South-South cooperation) ambao unabaki kuwa madhubuti na imara hadi leo.

ITEC ni sauti na nguzo inayoshamiri katika urafiki na ushirikiano wetu wa kimaendeleo baina ya India na Tanzania. Imekuwa ikiimarika sana katika miaka ya hivi karibuni, na idadi ya maafisa na wataalam wa kitanzania waliohudhuria mafunzo nchini India katika kipindi cha mwakajana kinazidi mia tano, ni mionganii mwa idadi kubwa sana katika bara la Afrika. Hongera sana.

Ni jambo linaloridhisha kwamba tumekuwa tukiimarisha na kudumisha ITEC na kulifanya jambo la maana sana. Hebu nitaje kwa uchache maendeleo yaliyofikiwa mwakajana nchini Tanzania. Kwanza, tunalenga zaidi maeneo ya kipaumbele kwa Tanzania kamavile afya, tehma, maji, na miundombinu. Pili, tulianzisha mafunzo ya awali ya e-ITEC katika masuala ya uanzilishi wa uchambuzi wa takwimu “Big Data Analytics” katika Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam (DIT), imefanywa na taasisi iliyoendelea sana nchini India.

Tatu, tumetoa shehena ya madawa kwa Bohari Kuu ya Madawa (MSD) zinazofikia thamani ya shilingi za kitanzania bilioni mbili, ikiwa ni jitihada za kusaidia juhudzi za Serikali ya Tanzania katika huduma za afya. Nne, tutaweka kambi kwa ajili ya uwekaji wa viungo bandia (miguu/mikono) kwa takriban watu wenye ulemavu miatano katika kitengo cha mifupa Muhimbili (MOI) mwezi mei mwaka huu.

Hebu nieleze kwa kifupi kwamba ushirika wa kimaendeleo baina ya India na Tanzania umeendelea kufanya vema sana mwaka jana. Miiongoni mwa miradi mikubwa sana ya India ambayo inaendelea hivisasa ni mradi wa usambazaji maji kutoka Ziwa Victoria hadi Tabora, Nzega, Igunga na vijiji themanini na tisa ambavyo vinapitiwa na mradi huo, kwa thamani ya shilingi za kitanzania bilioni mia sita. Miradi mingine miwili ya usambazaji maji katika jiji la Dar es Salaam, Chalinze na Zanzibar nayo pia inaendelea. Tumetoa ahadi zaidi kwamba shilingi za kitanzania trilioni moja nukta moja tano (Tsh1.15 trillion) zitatolewa kwa ajili ya usambazaji maji katika miji mingine ishirini na sita nchini Tanzania. Pia tumetoa mapendekezo ya kuwa na mpango wa uendeshaji masomo kwa njia ya mawasiliano (tele-education programme) katika vyuo vikuu vitano nchini Tanzania na matibabu kwa njia ya mawasiliano (tele-medicine programme) kwa hospitali tano, na nataraji kukamilisha makubaliano kuhusu masuala hayo katika muda mfupi ujao.

Kuna mengi ya kusherehekea kuhusu upamoja na ushirikiano baina ya India na Tanzania, ambao umekuwa mkubwa sana. Tunafarijika sana kwamba Mheshimiwa Naibu Katibu Mkuu, Profesa Mdoe ametoa muda wake na kuungana nasi katika sherehe hizi pamoja na wahitimu wa mpango wa ITEC. Napenda kutambua na kuthamini ushirikiano wa Serikali ya Tanzania, hasa Wizara ya Utumishi wa Umma pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje ya Tanzania katika mafanikio yetu ya pamoja katika ufanikishaji wa mpango wa ITEC kwa mafanikio na tija.

Sasa naomba kumualika Mheshimiwa Naibu Katibu Mkuu ili aweze kuchangia pamoja nasi fikra zake katika hafla hii.

Asanteni sana wote.